



Atakayesoma aya mbili za mwisho wa suratul Baqara zitamtosheleza

Imepokewa Kutoka kwa Abuu Masoud -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema:
amesema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-: "Atakayesoma aya mbili za mwisho
wa suratul Baqara zitamtosheleza".

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Ameeleza Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuwa atakayesoma aya mbili za mwisho katika suratul-Baqara usiku, basi Mwenyezi Mungu atamtosheleza na shari na kila lenye kuchukiza, na imesemwa: Zitamtosheleza na kisimamo cha usiku, na imesemwa: Zita mtosha na nyiradi zote, na imesemwa kuwa: Ni kiwango kidogo kinachoweza kumtosheleza mtu na kusoma Qur'ani katika kisimamo cha usiku, na imesemwa kinyume na hivyo, na huenda yote yaliyotajwa yanakusanywa na tamko hilo.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/6274>

النجاة الخيرية
ALNAJAT CHARITY

